SACRIFICE 316

## Dhabihu Iliyo Hai

*"Kwa hiyo, ndugu zangu, nawasihi kwa rehema zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu na inayompendeza Mungu, hii ndiyo ibada yenu yenye maana. Msifuatishe tena mfano wa ulimwengu huu, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu. Ndipo mtaweza kujaribu ili kuthibitisha mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yanayopendeza na kamilifu machoni pake."* Warumi 12:1-2

**Dhabihu yako.** Himizo hili la kutoa mwili wako kama *"dhabihu iliyo hai na takatifu"* mara nyingi hueleweka vibaya. Hata hivyo, himizo hili ni muhimu sana katika kukuonyesha njia sahihi ya kuwa zaidi ya Muumini wa Kristo tu. Mstari wa kwanza unampa kila Muumini changamoto ya kutoa dhabihu mahususi kwa Mungu baada ya wokovu. Mstari wa pili unatoa maagizo ya maisha unayopaswa kuishi baada ya kutoa dhabihu hiyo. Jinyenyekeze kwa Mungu kila siku kama sehemu ya kubeba msalaba wako kila siku, Luka 9:23. Hata hivyo, hilo si kusudi la Warumi 12:1. Amri yake ya *"itoeni miili yenu"* maana yake ni kufanya *uamuzi wa mara moja na kwa wakati wote* kujitoa, kujisalimisha, na kujinyenyekeza kikamilifu kwa Mungu. Huo si wokovu. Wokovu unatokana na dhabihu ya Kristo pekee. Hii ni tofauti. Hii ni dhabihu yako. Si dhabihu ya kila siku. Ni kutoa maisha yako bila masharti na milele kwa Mungu kama dhabihu iliyo hai, takatifu, na inayokubalika. Ni zawadi yako ya hiari ya kutoa nafsi yako kwa Mungu kwa ajili ya utukufu wake na ili akutumie bila kuwekewa mipaka yoyote.

**Kwa nini utoe dhabihu hii?** Ni kwa sababu ya rehema zake. Warumi sura ya 1-11 inaeleza rehema za Mungu. Warumi 12:1 inakuambia kile ambacho Mungu anataka ufanye kwa sababu ya rehema hizo. Warumi 12:2 inakupa mahimizo mawili kwa ajili ya maisha *baada ya* dhabihu yako. Rehema kuu za Mungu katika kukuokoa na kukutakasa zinaelezwa katika sura hizo kumi na moja za kwanza. Kwa hivyo, jitoe kwa Mungu. Atakubariki katika maisha haya na katika umilele. Hata hivyo, motisha sahihi ya dhabihu yako haiko mbele yako. Iko nyuma yako. Motisha yako sahihi inatokana na kile ambacho Mungu tayari amefanya. Fikiria Yesu anakuonyesha mikono yake yenye makovu ya misumari huku akisema, "Baada ya yote niliyokufanyia, nifanyie hili." Hiyo ndio maana ya Warumi 12:1.

**Kwa nini dhabihu ya mara moja kwa wakati wote?** Ni kwa sababu hiyo ndio maana ya maneno yaliyo katika Warumi 12:1-2. Vitenzi vilivyo katika *"msifuatishe"* na *"mgeuzwe"* katika 12:2 viko katika wakati uliopo. Hiyo inamaanisha ufanye mambo hayo sasa na uendelee kuyafanya maisha yako yote. Hata hivyo, kitenzi kilicho katika *"Itoeni miili yenu"* katika 12:1 hakiko katika wakati uliopo rahisi katika lugha ya Kigiriki. Katika Kigiriki, inamaanisha kitendo kimoja. Haimaanishi unapaswa kuendelea kukifanya. Inamaanisha ukifanye mara moja kwa wakati wote. Ni uamuzi thabiti wa kutoa nafsi yako kwa Mungu. Toa nafsi yako kama dhabihu kwake. Warumi 12:1 inahusu dhabihu yako. Inahusu wewe kujiweka milele kwenye madhabahu ya Mungu.

**Mifano Miwili.** Kumbukumbu la Torati 15:12-17 inatoa mfano wa suala hili. Mtumwa Mwebrania aliyeachiliwa huru angeweza kuamua *kwa hiari* na kwa kipindi cha *kudumu daima* kuwa tena mtumwa wa bwana wake. Uamuzi huo ulitokana na rehema za awali za bwana wake. Na ulisababishwa na upendo wa mtumwa huyo kwa bwana wake. Ulikuwa ni uamuzi wa kudumu. Mharazi ulitumika kutoboa sikio la mtumwa huyo kuonyesha kwamba yeye ni mtumishi wa bwana wake maisha yake yote. Utumwa huo ulikuwa ni uamuzi wa mtumwa mwenyewe. Hakulazimishwa kufanya hivyo. Ulikuwa ni uamuzi wa kudumu. Mfano mwingine uko katika dhabihu za wanyama za Agano la Kale. Ilikuwa ni lazima mnyama akubalike ili aweze kuwekwa kwenye madhabahu. Mnyama mgonjwa au mwenye dosari hakukubalika, Walawi 1-5. Hiyo inaonyesha mfano wa sehemu takatifu na inayokubalika ya dhabihu yako ya Warumi 12:1. Hali ya kufa ya mnyama anayetolewa kama dhabihu inaonyesha kwamba dhabihu hiyo ni ya kudumu. Hakuna mnyama aliyetolewa kama dhabihu angeondoka kwenye madhabahu yaliposhika moto. Hakuna kuhani aliyemchukua tena mnyama huyo mwishoni mwa siku ili ikiwezekana amtoe kama dhabihu siku nyingine. Dhabihu hiyo ilikuwa ni ya kudumu. Ukiondoa dhabihu yako ya Warumi 12:1 kutoka kwenye madhabahu yanaposhika moto, hiyo haikuwa dhabihu ya Warumi 12:1.

**Kurudia dhabihu yako.** Je, unapaswa kurudia dhabihu yako ya Warumi 12:1? Ndio, ikiwa dhabihu yako haikukubalika. Dhabihu ya Warumi 12:1 inahitaji kuwa hai, takatifu, na inayokubalika. Uko hai kwa sababu, baada ya kumwamini Kristo, *"ulipita kutoka mautini na kuingia uzimani,"* Yohana 5:24. Kuwa dhabihu takatifu ni jukumu lako. Wanyama wa Agano la Kale walihitaji kukubalika ili watolewe kama dhabihu. Hakuna mnyama angeweza kuwa mkamilifu. Lakini ilikuwa ni lazima awe bila ugonjwa, awe na afya, na bila dosari. Hiyo inaonyesha mambo mawili kuhusiana na dhabihu ya Warumi 12:1. Kwanza, dhabihu yako lazima isiwe na ugonjwa. Ugonjwa wa dhambi na kutenganishwa na Mungu lazima iponywe kwa njia ya wokovu. Ndio maana Warumi 12:1 imeandikiwa Waumini pekee (jambo linaloonyeshwa na maneno "ndugu zangu" katika mstari huo. Dhabihu ya mtu asiye Muumini haikubaliki kwa sababu dhabihu hiyo lazima itolewe *baada ya* wokovu na si *kabla* ya wokovu. Lazima uje kwa Yesu kabla hujamfuata. Ili uwe na uhakikisho na wokovu wako tembelea www.Gospel316.org. Sehemu inayotaja utakatifu inaonyesha kiwango kinachokubalika cha usafi wa kiroho katika maisha ya Muumini. Unapofikia kiwango hicho tu ndipo dhabihu yako ya Warumi 12:1 inkubalika kwa Mungu. *"Basi ikiwa mtu amejitakasa na kujitenga na hayo niliyoyataja, atakuwa chombo maalum, kilichotengwa na ambacho kinamfaa mwenye nyumba, kimeandaliwa tayari kwa kila kazi njema,"* 2 Timotheo 2:21. Huwezi kuwa mkamilifu. Hata hivyo, unaweza kujitoa ukiwa katika kiwango kinachotosha cha afya ya kiroho na utakatifu. Baada ya dhabihu yako iliyo hai na takatifu kukubalika na Mungu, huhitaji tena kuitoa tena. Hata hivyo, ikiwa dhabihu yako haikukubalika na Mungu kwa sababu ilikuwa ya muda mfupi au kwa sababu haikuwa takatifu, basi unahitaji kuitoa tena. Jitoe kama dhabihu ya kudumu, iliyo hai na takatifu. Kwa hiari yako, jifanye kuwa mtumwa wa kudumu wa Mungu. Usifanye hivyo kijuujuu. Ni uamuzi mzito sana baada ya wokovu. Baada ya dhabihu yako kukubalika, tekeleza Warumi 12:2 ambayo ni kuishi maisha yaliyogeuzwa yasiyofuata mfano wa ulimwengu huu kama mfuasi wa kweli wa Yesu Kristo. Baada ya yote aliyokufanyia, mfanyie hilo!

**Maisha baada ya kutoa dhabihu yako.** *"Msifuatishe tena mfano wa ulimwengu huu, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu. Ndipo mtaweza kujaribu ili kuthibitisha mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yanayopendeza na kamilifu machoni pake,"* Warumi 12:2. Mstari huu unatoa mahimizo ya jinsi ya kuishi baada ya dhabihu yako ya Warumi 12:1. Mahimizo hayo yako katika wakati uliopo kumaanisha uendelee kutofuata mfano wa ulimwengu huu na uendelee kugeuzwa kupitia mchakato unaoendelea wa kufanywa upya nia zako. Usifuate wala usikubali matendo ya dhambi ya ulimwengu huu. Usiache ulimwengu ushawishi utambulisho wako kama Muumini. Warumi 12:2 inakuhimiza *"kugeuzwa kwa kufanywa upya nia zako."* Neno la Kigiriki lililotafsiriwa kama *kugeuzwa* ndio neno lilelile lililotumika kwa Yesu katika Mathayo 17:2 na Marko 9:2 ambapo Biblia inasema Yesu *aligeuzwa.* Warumi 12:2 ni himizo la kugeuzwa kwa kufanywa upya (kurekebishwa, kubadilishwa kikamilifu ili kuwa bora zaidi) nia zako. Mabadiliko hayo (ambayo ni ya ajabu zaidi kuliko jinsi kiwavi anavyogeuka kuwa kipepeo) yanatimizwa unapojifunza Neno la Mungu na kuishi kulingana nalo. Toa dhabihu yako ya Warumi 12:1. Usikubali kulazimishwa kufuata mfano wa ulimwengu huu. Geuzwa kadiri unavyojifunza Neno la Mungu na kuishi kulingana nalo. Ndipo utatambua na kuishi kulingana na mapenzi ya Mungu.

**"Ndipo mtaweza kujaribu ili kuthibitisha mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yanayopendeza na kamilifu machoni pake."**

**Warumi 12:2**

---

*Dhabihu Iliyo Hai* © 2026 imeandikwa na John D. Morris III na kuchapishwa na Acts One Eight. Unaweza kuichapisha, kuinakili, kuichapisha mitandaoni, kuituma kupitia barua pepe, au kuituma kama ujumbe bila kubadilisha maudhui yake huku ukijumuisha kauli hii kikamilifu. Unaweza kujumuisha jina la huduma au kanisa lako au nembo yako kwenye sehemu ya juu ya ukurasa wa kwanza na uweke taarifa zako za mawasiliano juu ya mstari mzito ulio karibu na sehemu ya chini ya ukurasa wa pili. Mafundisho ya *Sacrifice316* yanatokana na Biblia pekee. Ipo ili kusaidia watu kukua kiroho zaidi ya kuwa tu Waumini wa Yesu. Unaweza kutuma barua pepe kwa Acts One Eight (katika lugha ya Kiingereza ikiwezekana) ukitumia anwani ifuatayo: Hello@Mail316.org. Huduma za utafsiri zimetolewa na www.ChristianLingua.com. *Dhabihu Iliyo Hai* inapatikana katika lugha 48 bila malipo kwenye www.Sacrifice316.org. (Not necessary to translate this segment as it talks abouth the English quotations of the Bible which don't apply in this translation). Nukuu za Maandiko katika tafsiri hii zimetolewa kutoka kwenye Biblia ya Neno.